UJIFUNZAJI WA BIBLIA WA WITO WA LAMBETH
KANISA SALAMA

UTANGULIZI

Nyenzo hizi za Kujifunza Biblia zimeandaliwa kama sehemu ya Awamu ya 3 ya Lambeth Conference na Miito ya Lambeth. Ujifunzaji huu wa Biblia unahusu Wito wa Lambeth kuhusu Kanisa Salama. Unaweza kusoma Wito wa Lambeth hapa.

Tunajua kwamba kufikiria na kuzungumza juu ya unyanyasaji kunaweza kufadhaisha kwa wale ambao wamepitia hali ya unyanyasaji au aina nyingine za ukiukaji, na pia kwa wale ambao wameona mtu wao wa karibu akiteseka kwa sababu ya unyanyasaji.

Tafadhali kuwa makini na hali hii na usihitaji washiriki wote wa kujifunza Biblia washiriki au wachangie. Wahimize washiriki wajitunze na wachukue muda au kuondoka ikiwa mazungumzo yanawasababishia maumivu au fadhaa. Ikiwa mtu ataelezea wazi kuhusu unyanyasaji kupitia mchakato huu, onyesha kujali kusaidia kwa huruma kama mchungaji na ufuate taratibu za kuripoti zilizopo katika dayosisi yako. Kwa mwongozo kuhusu michakato ya kuripoti, fikia rasilimali kwenye tovuti ya Tume ya Kanisa Salama kwa mwongozo zaidi na umsaidie mtu huyo kuripoti polisi, ikiwa inafaa.

JINSI YA KUTUMIA SOMO HILI

'Wito na Mwitikio' – Muundo wa Kujifunza Biblia

Kila moja ya Miito ya Lambeth hutolewa kwa Ushirika wa Anglikana – kukaribisha mwitikio. Ujifunzaji wa Biblia upo katika muundo wa 'Wito na Mwitikio'. Kila moja ya Masomo ya Kujifunza Biblia ya Wito wa Lambeth yatakualika kuchukua hatua tatu.

1. Sikia Wito
Chunguza pamoja Ujumbe mmoja wapo kati ya ujumbe mkuu wa Wito huu na uzingatie jinsi maandiko yanavyoweza kuongoza uelewa wetu wa ujumbe wa Wito wa Lambeth .

2. Sikiliza Maandiko
Soma na tafakari kuhusu vifungu vya Biblia vilivyochaguliwa kwenda sambamba na ujifunzaji huu.

3. Andaa Mwitikio
Elewa jinsi wewe binafsi unavyoweza kuitikia ujumbe katika Wito wa Lambeth na kuendeleza miongozo ya Kanisa Salama katika mazingira yako.

ANZA

1. Sikia Wito (Dakika 20)

Soma Wito wa Lambeth kuhusu Kanisa Salama hapa.
Tazama video fupi za rekodi za mafunzo kwa njia ya mtandao kuhusu mada husika ili upate muktadha.

Zingatia kwamba Wito wa Lambeth kuhusu Kanisa Salama unatangaza kwamba **Maandiko yanashuhudia upendo wa Mungu kwa wanadamu wote na kipaumbele kilichotolewa katika huduma ya Yesu kwa watoto, walio katika mazingira magumu na waliotengwa** (2.3).

Zingatia kwamba Wito unaangazia aina nyingi za matumizi mabaya ya mamlaka ndani ya jamii na kanisa. Wengi wa wale wanaonyanyaswa ni wanawake na wasichana: 'Vurugu zilizofanyika kwa wanawake na watoto katika mwili wa Kristo ni vurugu inayofanywa kwa mwili wa Kristo. Vurugu inakuwa na aina nyingi ikiwa ni pamoja naunyanyasaji wa kimwili, kifedha, kihisia, kisaikolojia, kiakili, kitamaduni, kingono na kiroho'. (2.3)

Kuna nyakati nyingi ambapo watu wanafanyiwa unyanyasaji badala kupewa upendo kutoka kwa familia ya wanadamu. Aina zote za vurugu na unyanyasaji zinaweza kusababisha madhara na mateso yanayoendelea kwa wale wanaonyanyaswa na wale walio karibu nao.

Chukua muda kukumbuka na kukiri kwamba sisi tulio kanisani hatutimizi wito wa kupendana kila wakati kama Mungu anavyotupenda.

Wakati mwingine washiriki wa kanisa na viongozi wa kanisa, makasisi na viongozi wa kawaida, huwanyanyasa na kuwadhuru wengine kanisani au katika familia zao wenyewe. Wito wa Lambeth unachukulia unyanyasaji huu kwa uzito na unatoa wito kwa makanisa yote katika Ushirika wa Anglikana kufanya vivyo hivyo.

Inaweza kusaidia kutumia muda kiasi katika maombi ya kimya kwa ajili ya makanisa yetu na kwa wale ambao wameumizwa na unyanyasaji ndani ya kanisa.

Unyanyasaji hauleti tu athari kwa mtu anayenyanyaswa. Una athari kwa familia zao, wenzao na jamii kwa ujumla. Unyanyasaji ndani ya kanisa unaweza kuwa na athari mbaya kwa jamii ya kanisa. Unaweza kuharibu imani kanisani na kwa Mungu.

Waombee wale wote ambao wameathiriwa na unyanyasaji. Tunaweza pia kujiombea wenyewe kwamba tuwe na ujasiri wa kusikiliza na kutenda ili kufanya makanisa yetu yawe mahali salama kwa wote.

2. Sikiliza Maandiko (20 minutes)

Soma Marko 5 mistari 21 hadi 34

Geukia kwenye Maandiko ili kutia nanga na kuimarisha tafakari hii, haswa kwenye huduma ya Yesu na wale ambao walitengwa na kudhulumiwa na jamii zao. Marko 5 mistari 21 hadi 34 ni kisa ambacho si tu chenye uchangamani na mabadiliko ya madaraka lakini kina mambo mengi ya kujifunza tunapofikiria maana ya kuwapenda wale wanaoteseka kwa kunyanyaswa.

Baadhi ya maoni juu ya kifungu hicho
Yesu anapoharakisha pamoja na Yairo kwenda kwa binti yake, ambaye ni mgonjwa sana, kisa hicho kinaelezea.

Yairo amemsihi Yesu aende kumponya binti yake. Umati unawazunguka wanapoharakisha kuelekea nyumbani kwa Yairo lakini Yesu ghafla akasimama na uangalia nyuso za watu waliokuwa wakimsonga. Kukawa na kimya, na Yesu anazungumza kwa mamlaka na huruma. ‘Ni nani aliyegusa mavazi yangu?’

Wanafunzi wanaona swali hilo ni la ajabu sana. Watu wengi wamemgusa Yesu muda mfupi tu uliopita, anaweza kuwa anamaanisha nini? Lakini kuna mwanamke mmoja ambaye anajua hasa anachomaanisha. Mwanamke huyo amekuwa akitokwa na damu kwa miaka 12. Mateso ya mwili na usumbufu wa ugonjwa huo hakikuw akitu kibaya zaidi katika ugonjwa wake.

Kwa sababu ya hali yake, alichukuliwa kuwa ni najisi na kutengwa na mahali pake pa ibada na jamii yake. Mwanamke huyo pia amedhulumiwa na kunyanyaswa. Tunasikia kwamba alikuwa amekwenda kwa kila daktari. Wamechukua pesa zake lakini bado hajapona. Kimsingi hali inazidi kuwa mbaya zaidi.

Huyu ni mwanamke ambaye amemalizi Kila kitu alichokuwa nacho. Lakini anajua Yesu alimaanisha nini alipouliza ni nani aliyemgusa. Alikuwa amekusanya nguvu zake zilizobaki na ujasiri kujipenyeza kwenye umati wa watu ili kumkaribia Yesu vya kutosha, aguse vazi lake, kwa matumaini makubwa kwamba angeponywa. Na aliponywa.

Kama linavyoonekana kuwa jambo la kushangaza, anajua kwamba mwili wake ulirejeshwa kikamilifu wakati vidole vyake viligusa kitambaa. Lakini sasa anaogopa. Anajua kwamba amekiuka miiko na mguso wake umemfanya Yesu kuwa najisi na kwa hivyo anatarajia kuhukumiwa. Anafikiria atoroke atoke kwenye umati. Lakini pengine kutokana na upole wa sauti yake, upole uliioonekana kwenye macho yake, tabasamu hafifu linaloonekana midomoni mwake linampa ujasiri anaohitaji ili abaki, na anatetemeka mbele yake, akificha uso wake.

Umati sasa umenyamaza, umevutiwa na kile kinachoendelea mbele yao. Yesu atashughulikaje na mtu huyu asiye na jina, mwanamke huyu aliyetengwa? Lakini hakuna kukemea na hakuna maneno makali. Labda Yesu anashuka chini na kumshika mkono mwanamke huyo, akimwinua asimame. Labda anauliza tena, akitazama machoni pake, kwa upendo na furaha. Ni nani aliyegusa vazi langu? Na labda anataja jina lake. Na tunaweza kufikiria wakati huo wa kuonwa kwa upendo.

Akiwa ametiwa moyo, anamwambia hadithi yake yote, si tu kuhusu tatizo lake la kimwili, lakini kile alichofanyiwa, jinsi alivyoitikia, ukweli wote wa kutisha, hukupa Yesu akisikiliza. Mbele ya jamii, ambayo ingemtenga, anasikiliza, na katika uwepo wake wa kusikiliza Yesu anarejesha zaidi ya afya yake ya mwili. Anarejesha heshima yake na nafasi yake katika jamii na kumwondolea aibu. Na bila kusema neno, anafichua udhalimu wa wale wanaosikiliza pamoja naye.

Kisha Yesu anazungumza. Anamwita mwanamke huyo ‘binti‘, neno la urafiki na kifamilia, ambalo linatuambia yeye ni wa nyumbani na anapendwa. Anathibitisha imani yake, imani ambayo imevumilia licha ya kutengwa na jamii ya waumini kwa zaidi ya muongo mmoja. Anazungumza maneno ya baraka, na wito: ‘Nenda kwa amani’, na kumrejesha katika utimilifu katika kila nyanja ya maisha yake. ‘Kuwa huru dhidi ya mateso yako’.

(Kim Barker, *Kanisa la Mungu kwa Dunia ya Mungu,* ukurasa za 98-99)

Maswali ya kujadili

- Ni nini kinachokuvutia zaidi kuhusu ambavyo Yesu anaingiliana na mwanamke huyu?
- Yesu hakuwa na haja ya kusimama. Mwili wa mwanamke huyo ulikuwa umeponywa alipogusa vazi lake. Kwa nini unadhani Yesu alichagua kusimama?
- Mwanamke huyu alikuwa amefanyiwa ukatili.
    - Waliomfanyia ukatili walikuwa ni akina nani?
    - Alifanyiwa ukatili kwa jinsi gani?
    - Ni kitu gani kilichomfanya awe katika mazingira ya kuwa mlengwa wa ukatili?
- Je, kisa hiki kinatupatia nini tunapofikiria kuhusu kazi ya Kanisa Salama?

3. Onyesha Mwitikio (Dakika 20)

Wito wa Lambeth unatuelekeza kwenye **upendo wa Mungu kwa wanadamu wote. Chukua muda kukumbuka** jinsi ambavyo umeuona upendo wa Mungu ama katika maisha yako mwenyewe au katika maisha ya wale wanaokuzunguka.

Fikiria kuhusu kifungu cha Biblia ambacho umejadili na kile tunachoweza kujifunza kutoka katika mfano wa Yesu.

Jadili na uamue jinsi unavyoweza kutenda kuhusu kile ulichojifunza kutoka kwenye hadithi hii, kanisani kwako au kazini au katika jamii kwa ujumla. Kanisa linawezaje kuonyesha upendo wa Mungu kwa wale ambao wamenyanyaswa au wananyanyaswa?

Jadili na uamue jinsi kanisa lako linavyoweza kuhakikisha kuwa linasikiliza na kuzingatia uzoefu wa wale ambao wamenyanyaswa.

Kanisa linawezaje kuwa na maarifa na ujuzi unaohitajika kujibu kwa huruma na mchakato wa haki wakati unyanyasaji unaripotiwa?

Tunapaswa kufanya nini ili kuhakikisha kuwa walio katika mazingira magumu wanalindwa na unyanyasaji unazuiwa?

Ikusanye timu ili msome hati ya *Kanisa Salama: Mwongozo wa Jinsi ya Kuanza*.

Iruhusu timu hiyo iongoze kanisa kuelekea kutumia Mkataba wa Usalama wa Watu ndani ya Makanisa ya Ushirika wa Anglikana na kutekeleza Miongozo, kuimarisha usalama wa watu wote, hasa watoto, vijana na watu wazima walio katika mazingira magumu, ndani ya majimbo ya Ushirika wa Anglikana.

Kwa makanisa yale ambapo hatua za Kanisa Salama/kulinda usalama tayari zipo, ni hatua gani inayofuata ambayo unahitaji kuchukua? Kazi ya Kanisa Salama haikamiliki kamwe.. Ni kazi inayoendelea kufanya makanisa yetu yawe salama kwa wote.

Maombi ya Kuhitimisha

Maombi kwa wale wanaoteswa na unyanyasaji

Kumpenda Mungu,
ambaye mwanawe alikuwa mwathiriwa na mshindi,
tunakulilia kwa ajili ya wale wanaoteswa na unyanyasaji:
kuwa pamoja nao katika machafuko na maumivu,
ponya majeraha ya mwili na akili,
vunja magereza ya hofu, kujishuku na kukata tamaa,
na kuwaimarisha wakabiliane na mstakabali wao kwa imani, tumaini na ujasiri.
Wafikie kwa upendo wako,
ili wapate kuwa wazima katika mwili, akili na roho,
kupitia mguso wa uponyaji wa Kristo anayeteseka.
Amina

Mungu, mkombozi na mpaji wetu,
tunawaombea waathiriwa wa ukatili, unyanyasaji na kupuuzwa.
Wape nguvu zako wasio na nguvu,
utimilifu wako kwa walio na utupu wa roho.
Waponye majeraha yao, waondoe hofu,
na uwarejeshee afya ya kweli.
Toa haya kupitia Yesu Kristo,
mwokozi aliyesulubiwa na kufufuka
ambaye yu hai na anatawala pamoja nawe na Roho Mtakatifu,
Mungu mmoja, milele na milele.
Amina.

Maombi kwa ajili ya wale wanaonyanyasa

Mhukumu wa dunia yote,
Mungu wa haki,
tunawaleta mbele yako wote wanaowanyanyasa wengine.
Geuza mioyo ya wenye ukatili wasiendee njia ya uovu.
Wajaze chuki dhidi ya uharibifu wanaofanya,
hivyo ukiwaleta kwenye toba ya kweli
na marekebisho ya maisha yao.
kwa ajili ya Yesu Kristo.
Amina.

Maombi kutoka sehemu ya *Maombi ya Mara kwa Mara* ya *Kitabu cha Maombi kwa ajili ya Australia.* Broughton Books. 1992.

NYENZO NYINGINEZO

Tembelea tovuti ya Lambeth Conference au angalia Karatasi ya Taarifa kuhusu rasilimali na mawazo yanayoambatana na Masomo haya ya Biblia, kwa maoni na mapendekezo zaidi.

Katika kila awamu ya Safari, unaalikwa kushiriki jinsi
Wito wa Lambeth ulivyo kwako katika muktadha wako. Unaweza kuchagua kushiriki sala, picha, ushuhuda mfupi au hadithi, maelezo kuhusu moja ya miradi yako.

Tafadhali shiriki kupitia tovuti yetu:
https://www.lambethconference.org/phase-3/share-your-story/

Au wasiliana nasi kupitia mitandao ya kijamii:
Facebook: /LambethConference
Instagram: /LambethConference
X: @LambethConf